JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI YA KINGUGI
S.L.P 46169 DAR ES SALAAM, SIMU – 0658413060

KUMB.NA.KING/SS/VOL.JI/2020.

TAREHE_____

JINA LA MWANAFUNZI _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINGUGI WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2021

UTANGULIZI

Nafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha KWANZA katika shule ya sekondari Kingugi mwaka 2021. KARIBU SANA.

Shule ya sekondari kingugi ipo katika wilaya ya Temeke. Eneo la Mbagala katika kitongoji cha Kingugi kwa simba. Ukifika Mbagala Zakhemu kuna kituo cha daladala ziendazo Kingugi kwa Dumba . Ukipanda shuka kituo cha mwisho Kingugi kwa simba, zinapogeuzia daladala, ukifika hapo ulizia mahali shule ilipo, umbali wa kama robo kilometa.

Shule ya sekondari ipo karibu na ofisi ya serikali ya mtaa wa Kingugi au kituo kidogo cha polisi. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 wewe unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/01/2021 kwa ajili ya utabulisho wa awali, (Orientation course).

1.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.01.0 SARE YA SHULE

Sare ya shule itakuwa kama ifuatavyo:

WAVULANA

I. Suruali mbili (2) kitambaa rangi ya Ugoro, estim na 1 (kitambaa kimeambatanishwa}Upana wa suruali chini usipungue nchi 17.
II. Mifuko ya mbele na nyuma izungushiwe kitambaa cha shifoni rangi ya blue bahari (light blue).
III. Shati mbili (2) tetroni mikono mifupi (Sharti fupi sana haziruhusiwi)

IV. Viatu vya ngozi nyeusi, visiwe na visigino virefu,wala visiwe vya wazi na viwe vya kamba (Raba hazitakiwi, migogo, yebo yebo na mfano wake)
V. Soksi nyeusi
VI. Mkanda wa ngozi Mweusi wa Suruali

NB:

- Suruali ya Mwanafunzi isiyotimiza vigezo itachanwa.
- Mwanafunzi atakae vaa viatu visivyoruhusiwa bila kibali cha mkuu wa shule atapokonywa, na hatorudishiwa.
- Mikanda ya suruali ya kitambaa/ Tambi n.k haziruhusiwi.

WASICHANA

I. Sketi mbili (2) kitambaa rangi ya Ugoro, mshono: linda boksi estim na. 1 (Aina ya kitambaa kimeambatanishwa). Kwa wanaovaa HIJAB sket ifike kwenye vifundo vya miguu.
II. Nchi mmoja Kutoka chini, Sketi izungushiwe kitambaa cha shifoni cha blue bahari size ya kati (Light blue).

III. Shati mbili (2) nyeupe tetroni mikono mifupi, (Shati fupi na za kubana haziruhusiwi) kwa wanaovaa HIJAB:-
  - Nusu kanzu isabane.
  - Kitambaa kiwe tetroni, vitambaa vya mipara haviruhusiwi.
  - Nusu kanzu iwe ndefu ivuke kiuno ifike katikati ya mapaja, nusu kanzu fupi haziruhusiwi kabisa
IV. Viatu vya ngozi nyeusi, visiwe na visigino virefu,wala visiwe vya wazi na viwe vya kamba (Raba, Bajaji hazitakiwi). Mwanafunzi atakae vaa viatu visivyoruhusiwa bila kibali cha Mkuu wa shule atapokonywa, na hatorudishiwa
V. Begi la ngozi nyeusi la kubebea vitabu mgongoni (school bag), hairuhusiwi wanafunzi kubeba madaftari pasi na begi.
VI. Soksi nyeupe ndefu (stocking) hadi chini ya magoti

NB i: Uvaaji wa hijabu ni hiari kwa wanafunzi wa kike na kanuni za uvaaji wa HIJAB zizingatiwe kama zilivyo

ii. Nguo za baridi ni sweta rangi ya kahawia shingo V kifuani (makoti, majaketi, vizibau, haviruhusiwi)

1.0 Sare za michezo

Unatakiwa kuwa na sare za michezo kama ifuatavyo

a. Wavulana: Seti mbili za jezi,moja rangi ya bluu na nyingine nyekundu (fulana na bukta yake).
b. Wasichana: Seti mbili za jezi,moja rangi ya bluu na nyingine nyekundu(fulana na suruali ya traki)

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa katika nakala utakayopewa yenye sheria na kanuni za shule.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU

4.1 unatakiwa kuwa na vifaa vyako binafsi kwa ajili ya matumizi mbalimbali hapa shuleni kama vile

i. Madaftari yasiyopungua 12 ukubwa saizi ya kati
ii. Mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical sets)
iii. Mathematical table (four figure) moja
iv. Peni,rula,kifutio na penseli

4.2 vilevile utatakiwa

a. Kuchukua fomu maalumu kwa ajili ya uchunguzi wa afya yako,(Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Daktari wa hospitali ya serikali tu na utairejesha kwa Mkuu wa shule.
b. Kujaza fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi , mkataba wa utiifu, kutoshiriki migomo fujo na makosa ya jinai.
c. Mzazi pia atajaza kwa kukiri kukubaliana na sheria za shule, na maelekezo yatakayotolewa na shule.

unatakiwa kusoma kwa makini sana maelekezo na maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NAKUKARIBISHA SANA KATKA SHULE HII

_____

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAISI – TAMISEMI
SHULE YA SEKONDALI KINGUGI

FOMU YA KUANDIKISHWA

A. IJAZWE NA MWANUFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi _____
2. Uraia _____
3. Dini _____
4. Tarehe ya kuzaliwa _____
5. Shule ya msingi aliyotoka _____
6. Mwaka wa kumaliza shule iyo _____

Picha ya Mwanafunzi ya hivi Karibuni akiwa amevaa shati la shule

B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la mzazi/mlezi _____
   Kama ni mlezi, uhusiano ni (mjomba,babu,kaka nk) _____
2. Anuani kamili mjini DSM _____
3. Sehemu anayoishi _____
4. Mtaa _____
5. Namba ya nyumba _____
6. Namba ya simu ya haraka _____
   - Ya nyumbani (land line) _____
   - Ya mkononi (mobile) _____

   (namba ya simu inayopatikana. Kama zipo mbili anadika zote)

   - Ya ofisini _____

Picha ya Mzazi/Mlezi

C. MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

- Jina la mwajiri na idara _____
- Anwani yake _____
- Nambari ya simu _____
- Kazi ya mzazi/mlezi(Meneja,Karani,Daktari,Mfanya biashara n.k)_____

D. SOMO LA DINI

Mimi _____ ambaye ni mlezi wa mwanafunzi _____kidato cha _____ ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya _____ dhehebu la _____siku ya kipindi cha dini akiwa shuleni Kungugi Sekondari.

_____

SAHIHI YA MLEZI/MZAZI

FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KINGUGI
S L P 46169.
DAR ES SALAAAM.
TAREHE……

KWA MWANAFUNZI.

Mimi _____(jina kamili) ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha _____mwaka _____katika Shule ya Sekondari Kingugi.

Naahidi kwamba :

1. Nitatii sheria za shule kama nilivyozisoma
2. Nitafanya bidii katika masomo, kazi na shughuli zote za shule
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali bila kutia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza malighafi.
4. Nitakuwa mwanafunzi mkakamavu na mwenye ari ya juu ya mwenendo safi wakati wote,nje na ndani ya shule ili kutunza sifa ya shule.
5. Sintoshiriki au kuanzisha migomo,fujo na makosa ya jinai

"EE MUNGU NISAIDIE"

_____

SAHIHI YA MWANAFUNZI

KWA MZAZI/MLEZI

Mimi _____

Naahidi kwamba

1. Nitampatia mwanangu mahitaji yote ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika na shule katika kumlea mwanangu
3. Nitafatilia mwenendo wa kimasomo wa mwanangu shuleni na nyumbani na kutoa taarifa shuleni nitakapobaini mwenendo kinyume cha masomo.
4. Nakubaliana na kanuni na sheria za shule zote kwani zitamletea mwanangu maadili mema ya kitanzania
5. Nitaitikia wito wowote kufika shuleni iwe nimetumia ujumbe kwa barua simu au nimeletewa taarifa ya mdomo na mwanangu kutoka shuleni.

Ahsante,

_____

SAHIHI YA MLEZI

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE PRIME MINISTER'S OFFICE – RALG

KINGUGI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 46169
DAR ES SALAAM
DATE: _____

MEDICAL OFFICER IN CHARGE

_____HOSPITAL/DISPENSARY
P.O.BOX _____

REF; REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Name of student _____

Please, examine the above named student as to her fitness to admission in the school in the following common diseases/problems.

Put a tick ( ) or cross (x) where appropriate in the right column.

Pregnancy	
Asthma	
Sight	
Diabetes	
Worms (stool)	
Epilepsy	
Tb (tuberculosis)	
Heart diseases	
Yellow fever	
U.T.I	
Any physical defects/disability	

CERTIFICATION

I (named) _____
medical officer/Doctor in charge that the named above has been examined and
Consider that she/he is physical FIT for admission.

KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

1. MAKOSA HAYA YANAWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE.
   i. Utumizi wowote wa madawa ya kulevya ikiwa ni Pamoja na kuuza au kusambaza.
   ii. Kupata ujauzito.
   iii. Kudharau nembo za serikali kama vile Wimbo wa Taifa, Fedha, Bendera, Fedha n.k.
   iv. Utoro, Mwanafunzi akifikisha siku 90 bila kuhudhuria shule atakuwa amejifukuzisha shule. Hata hivyo sheria hii iko kwenye marekebisho.
   v. Kuhamasisha au kuanzisha mgomo shuleni.
   vi. Kupiga shuleni kwa sababu yoyote ile.

2. ZINGATIA YAFUATAYO
   1. Unatakiwa kuwahi mahali popote pale unapotakiwa
   2. Unatakiwa kuhudhuria shuleni vipindi vilivyopangwa kwenye ratiba ya shule
   3. Unatakiwa kufanya mazoezi yote ya darasani na mitihani inayotolewa shuleni na itokayo nje ya shule kitaratibu
   4. Unatakiwa kuwa mfano bora wa nidhamu na tabia njema kwa kuwaheshimu walimu,wafanyakazi wasio walimu,watu wotw wakubwa kwa wadogo na wanafunzi wenzio popote pale. Ni marufuku kusema uongo
   5. Unatakiwa kuvaa vazi rasmi la shule linalotakiwa kwa wakati husika. (shati na suruali/sketi) siku zote
   6. Nywere za mwanafunzi zinatakiwa kuwa fupi na si ruhusa kunyoa vipara au mitindo aidha si ruhusa kwa wasichana kusuka nywele, zikatwe.
   7. Si ruhusa kwa mwanafunzi kuingia darasani na vyakula vya aina yoyote au vinywaji wala kutafunatafuna
   8. Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kupatikana katika hali ya ulevi ndani na nje ya shule aidha si ruhusa kuonekana

katika nyumba za starehe pamoja na nyumba za kulala wageni (guest houses)

9. Si ruhusa kwa mwanafunzi kutoka maeneo ya shule bila kibali cha mwalimu wa zamu,darasa au makamu mkuu wa shule muda wa shule
10. Wageni wa wanafunzi wote wakifika shule ni lazima wapiti ofisini kwa walimu.
11. Lugha ya mawasiliano muda wote ukiwa hapa shuleni ni Kiingereza.
12. Unatakiwa kuwa mtunzaji wa mali za shule na binasfi na si ruhusa kuharibu kifaa chochote kwa makusudi
13. Si ruhusa kwa mwanafunzi kutumia madawa ya kulevya kama vile bangi.
14. Mwanafunzi anatakiwa kujitunza na kuwa msafi muda wote kimwili,kimavazi na kiroho
15. Si ruhusa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu (matusi) wakati wote akiwa nje na ndani ya shule
16. Hairusiwi kuchafua sehemu mbalimbali kwa kuweka maandishi kama vile kwenye kuta, kwenye vitabu na mali za shule nk
17. Ni marufuku kabisa kugoma kufanya adhabu yoyote iliyotolewa na mwalimu yeyote au kiongozi yoyote wa serika ya mwanafunzi.
18. Ni marufuku kushiriki katika ugomvi na namna yoyote ile iwe kwa maneno au kupigana na mwanafunzi mwezio au mtu mwingine yeyote Yule

19. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kufanya biashara ya aina yoyote ile ndani ya shule au Darasani isipokuwa kwa ruhusa ya Mkuu wa Shule
20. Ni kosa kubwa kutoa habari za shule nje au kwa waandishi wa habari bila ruhusa ya mkuu wa shule.
21. Wizi, uporaji wa ndani au nje ya shule ni kosa la kumfukuzisha mwanafunzi shule.
22. Si ruhusa Mwanafunzi kumiliki simu.

NB: Mzazi/Mlezi hana budi kuyasoma na kuyaelewa maelekezo haya ya kujiunga na shule kwa sababu yatatumika kama mkataba baina ya Mzazi/Mlezi na Shule.